

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA ARUSHA:
Anwani ya simu "REGCOM"
Simu Na. 2545608/2544950/2544802
Fax Na: 2545239 / 2544386
Barua Pepe: ras@arusha.go.tz
Barua Pepe: ras.arusha@tamisemi.go.tz
Tovuti: www.arusha.go.tz



OFISI YA M KUU WA MKOA,
S.L.P. 3050,
ARUSHA.

24 Juni,2020

TAARIFA KWA UMMA
VIONGOZI WATAKIWA KUFANYA KAZI KWA KUSHIRIKIANA

Mkuu wa Mkoa wa Arusha Mheshimiwa Idd Hassan Kimanta, amewataka viongozi wote wa Mkoa wa Arusha kufanya kazi kwa kushirikiana kwani umoja ni nguvu.

Kimanta ameyasema hayo alipokuwa akizungumza na viongozi mbalimbali wa Mkoa wa Arusha wakiwemo Wakuu wa Wilaya, Wakurungenzi na Makatibu Tawala wa Wilaya zote za Mkoa baada ya kupokelewa rasmi kama Mkuu wa Mkoa wa Arusha.

Amesema ushirikiano na uvumilivu ndio silaha muhimu katika kuongoza na kuleta maendeleo katika jamii.

Amesisitiza kuridhika na vile walivyonavyo ili kuleta heshima katika kutekeleza majukumu ya kila umoja kwa nafasi yake.

Pia, amewataka kusimamia miradi yote ya maendeleo ambayo serikali imetoa fedha zake kwa lengo la kuleta maendeleo kwa wananchi na nchi kwa ujumla.

Imetolewa na;

Kitengo cha Habari na Mawasiliano,
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa
Arusha.